

HALMASHAURI YA WILAYA YA KARAGWE

Simu: 028-2227148
Fax: 028-2227140
Tovuti: www.karagwedc.go.tz



S. L. P. 20,
KARAGWE

12/02/2019

TANGAZO KWA WANANCHI WOTE KUHUSU ZOEZI LA UENDESHAJI WA CHANJO KWA NG'OMBE DHIDI YA UGONJWA WA CHAMBAVU NA KIMETA

Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe inatarajia kuanza zoezi la chanjo kwa ng'ombe dhidi ya ugonjwa wa Chambavu na Kimeta lengo la chanjo hii ni kutoa kinga kwa ng'ombe dhidi ya magonjwa hayo mawili yaani chambavu na Kimeta. Zoezi hili litaanza rasmi tarehe 20/02/2019 na kuhitimishwa tarehe 30/03/2019, kila siku kuanzia saa 1.00 asubuhi hadi saa 10.00 jioni, isipokuwa siku ya Jumapili tu. Mfugaji atachangia **T.Shs 1,500/=** (Elfu Moja n Mia Tano Tu.) kwa kila ng'ombe kwa chanjo zote mbili.

Zoezi hili la chanjo litahusisha Wilaya nzima ya Karagwe na Ratiba ni kama ifuatavyo;

TIMU NAMBA 1	TAREHE	TIMU NAMBA 2	TAREHE
Rugu, Nyaishozi, Ihembe na Nyakasimbi	20/02/2019 hadi 05/03/2019	Vitalu (block). (1).Kiteto Agro Bussiness Ltd, (2). Kagera Suger (Block 2, 3, 4, 6, 8) (5). Abakundaine Trustee,(5). Mtebu Investiment Co. Ltd,(9). Charles Burchard Lwabutondogoro, (10). Edivedius Rutta Kassano, (11).Laurian Kasenene Rubega, (12). Bugengele Farm, (13). MCI Worldwide Ltd (14). Kagango Dairy Farm	20/02/2019 hadi 30/02/2019

TIMU NAMBA 1	TAREHE	TIMU NAMBA 2	TAREHE
Bweranyange Nyakabanga, Nyakakika na Kibondo	06/03/2019 hadi 20/03/2019	Rugera, Kihanga, Ndama, Kayanga na Bugene.	01/03/2019 hadi 10/03/2019
Kamagambo Nyabyonza na Kiruruma	21/03/2019 hadi 30/03/2019	Chanika, Kanoni, Igurwa na Kituntu.	11/03/2019 hadi 20/03/2019
		Nyakahanga, Ihanda, Chonyonyo	21/03/2019 hadi 30/03/2019

Vibanio vya kutolea chanjo kwa kila kata, mtajulishwa na uongozi wa kata husika.

Zoezi hili linafanyika kwa mujibu wa sheria ya uzuiaji magonjwa ya mwaka 2003. Katika sheria ya magonjwa ya mifugo No. 17 ya mwaka 2003 kipengele 62 (1b) ukurasa wa 33. Imeeleza wazi, mtu yeyote atakwenda kinyume na matakwa ya sheria hii, atatozwa faini isiyopungua Laki Tatu **(300,000.00)** na Isiyozidi Laki Tano **(500,000.00)** au **kifungo cha miezi sita jela** au vyote kwa pamoja **(faini na kifungo)**

Upatapo tangazo hili mjulishe na mwingine

Imetolewa na

Godwin M. Kitonka
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
KARAGWE